

# BARAZA LA HABARI TANZANIA



S.L.P 10160, Dar es Salaam, Tanzania  
Simu: +255-22-2775728/2771947  
0732998310

Simu ya mkononi: +255-784-314880  
Nukushi: +255-22-2700370,0732991521  
Barua pepe: media@mct.or.tz  
Tovuti: <http://www.mct.or.tz>  
Zanzibar Office: P.O.Box 3490,  
Tel/Fax: +255-24-2239728  
Email: mctz@mct.or.tz

P.O.Box 10160, Dar es Salaam, Tanzania  
Tel: +255-22-2775728/2771947/  
0732998310

Mob: +255-784-314880  
Fax: +255-22-2700370,0732991521  
Email: media@mct.or.tz  
Website: <http://www.mct.or.tz>

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

MCT/4.2/004/2011

### Baraza la Habari laonya kuhusu uandishi wa masuala ya dini usiozingatia maadili

**Tarehe: 19/05/2011** Baraza la Habari Tanzania (MCT) limebaini kwa masikitiko mwenendo unaojitokeza wa kuripoti masuala ya dini bila kuzingatia maadili.

Baraza linapenda kuwakumbusha waandishi na wahariri kuwa masuala ya imani yana unyeti unaopaswa kuzingatiwa katika kuripoti, ili kuepuka upotoshaji unaoweza kuleta uchochezi na chuki katika jamii.

Kumekuwa na uandishi usiozingatia uhalisia (objectivity), ulinganifu (balance) na umahsusi (specificity) na badala yake kuchukua mfumo wa kuegemea upande mmoja (bias) na kufanya majumuisho (generalisation) yasiyotokana na ukweli uliothibitishwa na mwandishi.

Mapungufu hayo ya kiweledi yamesababisha habari nyingi kuwa potofu na chonganishi.

Weledi hautaki kwa mfano gazeti kumhoji sheikh mmoja au kadhaa au askofu mmoja au kadhaa na kutoka na vichwa vya habari vinavyosema "**Waislamu wataka . . .**" au "**Wakristu wataka . . .**" Ikiwa ni mawazo ya kiongozi fulani wa kidini ni bora itajwe hivyo. Dhehebu linaweza kuhusishwa tu ikiwa yeye ni msemaji rasmi na anaongea kwa niaba ya dhehebu hilo.

Vichwa vya habari kama "**Maaskofu wamng'oa Naibu Meya Arusha**" huku kukiwa hakuna ushahidi wowote ndani ya habari yenyewe unaoashiria kuwa kujiuzulu kwa huyo Naibu Meya kulitokana na shinikizo la maaskofu ni upotoshaji unaoweza kusababisha chuki.

Mbaya zaidi ni pale kesho yake gazeti jingine linapowafuata masheikh na kuwaomba kauli yao kuhusiana na kung'olewa kwa Naibu Meya "kulikofanywa na maaskofu". Ni wazi hapa kuna hatari ya wanahabari kugeuka wachonganishi.

Pamewahi pia kuchapishwa kichwa kilichosema "**Masheikh wawaonya maaskofu**". Hii ni hatari!

Habari nyingine ilidai bila uthibitisho wowote kuwa waumini wa Kanisa Katoliki wametengwa na Kanisa hilo kwa kujihusisha na chama fulani cha siasa. Viongozi wa Kanisa hilo hawakuhojiwa.

Na hata hivi karibuni tu gazeti moja liliandika: “ **Waislamu: Osama hajafa – wadai kuzikwa haraka ni dalili za kuficha ukweli .**”


Hivi kweli maoni kwamba Osama hajafa yalikuwa ni maoni ya Waislamu wote nchini? Na je, baada ya vyombo vya habari kuripotiki siku kadhaa baadae kwamba Al-Qaeda wenyewe wamekiri kuwa Osama kafa, gazeti hilo halijisikii vibaya kwamba limewasababishia dhahaka Waislamu wote bila uhalali wowote lilipowasingizia kwamba wamesema Osama hajafa?

Gazeti lingine nalo hivi karibuni lilinukuu maoni ya mchungaji mmoja anayedaiwa kupinga ukaguzi wa mahesabu ya makanisa na kuandika kichwa kilichosema “**Makanisa yakataa kukaguliwa na serikali**”.

Baadae katibu wa makanisa yaliyotajwa alinukuliwa akisisitiza kuwa yale yalikuwa mawazo binafsi ya mchungaji huyo.

Kifungu 1.9 cha kanuni za maadili kwa wahariri (uk.5) kinazuia ubaguzi na kinasisitiza: “ Hakikisha habari hazilengi wala kutoa nafasi kwa ubaguzi wa kijinsia , dini makundi ya watu wachache, umri, kabila . . .” Kuhusu dini kifungu 1.14 (uk. 6) kinaelekeza: “Zungumza na mashirika ya dini, yape haki sawa na heshima yanayostahili kwani hadhi za wawakilishi, viongozi, waumini na imani zao zinapaswa kuheshimiwa na kuthaminiwa”.

Kwa misingi hiyo Baraza la Habari linapenda kuwakumbusha waandishi na wahariri kuepuka uandishi wa majumuisho yasiyokuwa na uthibitisho au uhalali; na pia uandishi unaoweza kuchochea chuki baina ya waumini na serikali. Jambo hili ni muhimu sio tu kwa manufaa ya taaluma bali pia kwa kulinda amani na umoja katika Taifa.

  
Kajubi D. Mukajanga  
**Katibu Mtendaji**